CHAMA CHA MAPINDUZI

MWELEKEO WA SERA ZA CCM KATIKA MIAKA YA 2000 HADI 2010

Imetolewa na:-

Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM
Agosti 2000

YALIYOMO **UKURASA**

1. SURA YA KWANZA
   Utangulizi ..... 2 - 6

2. SURA YA PILI
   Kujenga Msingi wa Uchumi wa Kisasa wa
   Taifa Linalojitegemea ..... 7 - 16

3. SURA YA TATU
   Mikakati ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Wananchi ..... 17 - 21

4. SURA YA NNE
   Sekta ya Huduma za Jamii ..... 22 - 24

5. SURA YA TANO
   Utawala Bora, Demokrasia na Madaraka ya Wananchi ..... 25 - 28

6. SURA YA SITA
   Maeneo Maalum 29

7. SURA YA SABA
   Utamaduni na Michezo 30

8. SURA YA NANE
   Siasa ya Mambo ya Nje ..... 31 - 32

9. SURA YA TISA
   Ulinzi na Usalama 33

10. SURA YA KUMI
    Chama Cha Mapinduzi na Umoja wa Taifa; Amani na
    Utulivu, na Mapinduzi ya Uchumi 34-37

MWELEKEO WA SERA ZA CHAMA CHA MAPINDUZI KATIKA MIAKA YA 2000 HADI 2010

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

Mwelekezo wa Sera za CCM katika Miaka ya Tisini

1. Mkutano Mkuu wa Nne wa Kawaida wa Chama Cha Mapinduzi uliofanyika mjini Dodoma mwezi Desemba, 1992 ulitangaza Mwelekeo wa Sera za CCM katika Miaka ya Tisini. Hii ni dira ambayo ingekiongoza Chama chenyewe na Serikali zake katika kuainisha majukumu, kupanga malengo na mikakati ya utekelezaji. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 1995 iliandaliwa kutokana na maudhui ya Mwelekeo huo.

2. Utekelezaji wa maelekezo ya Mwelekeo haukuwa wa mafanikio makubwa katika nusu ya kwanza ya miaka ya tisini. Mapungufu haya yalitokana na sababu kubwa mbili. Kwa upande mmoja kipindi hiki kiliambatana na nchi kuingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa. Chama na Serikali zake ilibidi zielekeze nguvu na muda mwingi kwenye hatua za kuunda mazingira yanayowezesha mfumo wa vyama vingi vya siasa kushamiri na pia kuyadhibiti mazingira hayo ili yasichafue hali ya amani, usalama, umoja wa taifa na mshikamano wa wananchi ambavyo vimejengeka nchini kwa miaka mingi. Kazi hii ilifanyika vizuri na kuweka msingi uliowezesha Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 1995 kufanyika katika mazingira ya amani na utulifu, uhuru na haki nchini kote.

3. Kwa upande wa pili, katika kipindi cha mwanzo cha miaka ya tisini Tanzania iligubikwa na matatizo makubwa ya kiuchumi: makusanyo madogo ya mapato ya serikali, mfumko wa bei wa zaidi ya asilimia 30, viwango vya juu vya riba na kiasi kidogo cha akiba ya fedha za kigeni kikilinganishwa na kiasi cha mahitaji ya kulipia bidhaa za kutoka nje. Hali mbaya ya menejimenti ya uchumi pamoja na kuongezeka kwa uozo wa rushwa kwa ujumla kulisababisha mvutano kati ya nchi yetu na wahisani. Hatimaye kuanzia mwaka 1994 hadi 1995 vyombo vya fedha vya kimataifa na nchi wahisani viliamua kusimamisha misaada na mikopo kwa Tanzania hadi hatua thabiti za kuendesha uchumi na kudhibiti rushwa zingedhihirika.

4. Pamoja na matatizo hayo ya kiuchumi, wananchi waliendelea na kuongeza juhudi za kujitatulia matatizo yao ya maendeleo katika sekta ya huduma za jamii. Katika kipindi hiki shule nyingi za msingi na za sekondari zilijengwa. Moyo huo wa kujenga taifa, ulijitokeza pia katika eneo la afya ambapo zahanati nyingi zilijengwa hasa vijijini.

5. Kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu wa Rais wa Jamhuri na Rais wa Zanzibar, Wabunge na Wawakilishi kulileta msisimko mkubwa wa kisiasa nchini. Kuundwa kwa Serikali ya Jamhuri ya awamu ya tatu kwa msingi wa ahadi za CCM kwa wananchi zilizoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 1995 kulitoa matumaini mapya kwamba kazi ya kujenga na kuendeleza uchumi imara na huduma za jamii endelevu itakidhi matarajio ya walio wengi.

6. Katika kipindi hiki cha pili cha miaka ya tisini (yaani 1996-2000) Serikali zimeweza kuurekebisha uchumi na kuurudisha kwenye reli. Mfumko wa bei umedhibitiwa na sasa umeshuka hadi kufikia asilimia sita (6%) na unatarajiwa kushuka zaidi; mapato ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yameongezeka zaidi ya maradufu kati ya Novemba, 1995 na Mei 2000; viwango vya riba vimeshuka; akiba ya fedha za kigeni imeongezeka kufikia inayotosheleza kulipia bidhaa za kutoka nje za miezi mine, kiwango kinachokubalika kimataifa.

7. Juhudi na hatua ambazo Serikali ya awamu ya tatu imeonyesha na kuchukua zimeunda mazingira mapya ya Tanzania. Kwa kurekebisha uchumi wa taifa, na kuimarisha menejimenti ya uchumi huo, wahisani wamelazimika kurudisha ushirikiano wao na Tanzania wa kifedha na kiuchumi. Mipango ya Serikali ya kuinua uchumi na kujielekeza kwenye vita dhidi ya umaskini, jambo ambalo linaungwa mkono na jumuiya ya kimataifa, imeipa nchi yetu heshima ya kutambuliwa kuwa ina uongozi makini na unaowajibika. Ndiyo maana nchi yetu imeteuliwa na jumuiya ya kimataifa kuwa miongoni mwa nchi zinazostahili kupunguziwa/kufutiwa/kusamehewa madeni.

8. Mafanikio haya yameongeza ari ya wananchi ya kushirikiana na Serikali zao kwa kufanya kazi za kujenga taifa. Hivyo wameendelea kujenga madarasa, nyumba za walimu n.k. kwa kujitegemea. Kasi ya ujenzi wa shule za serikali za wananchi imeongezeka. Vivyo hivyo, zahanati nyingi zaidi zimeendelea kujengwa katika kipindi hiki. Kuongezeka kwa fedha zinazotengwa na serikali kwa ajili ya barabara za vijijini kumewafanya wananchi wajitokeze kwa wingi kuimarisha barabara zao.

Malengo Makuu ya Mwelekezo wa Sera wa Miaka ya Tisini

9. Tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM ya 1995 inaonyesha kuwa Serikali zote mbili, ya Muungano na ya Zanzibar, zimefanikiwa kutekeleza ahadi nyingi zilizotolewa na Ilani hiyo. Pale ambapo malengo hayakufikiwa wananchi wameelimishwa juu ya sababu za hali hiyo.

10. Hata hivyo, tathmini sahihi ya utekelezaji wa Ilani inayokumbatia masuala ya ujenzi wa uchumi na uboreshaji wa huduma za jamii na maisha ya wananchi haiwezi kuishia kwenye kuorodhesha ahadi zilizotekelezwa na zile ambazo hazikutekelezwa tu, bali lazima iambatane na uchambuzi wa uwezo wa ziada ambao Serikali imejijengea katika kipindi kinachohusika utakaoiwezesha kuwa na nguvu zaidi za kusukuma maendeleo ya uchumi na jamii ya nchi katika kipindi kinachofuata. Serikali ya CCM ya awamu ya tatu imefanikiwa kukidhi kigezo hiki pia. Serikali imefanikiwa kuongeza mapato yake toka wastani wa Tsh. 27bn/- kwa mwezi mwaka 1995 hadi wastani wa Tsh. 55bn/- kwa mwezi mwaka 2000 na mapato hayo yanaonyesha mwelekeo wa kuongezeka. Pili, Serikali imefanikiwa kuvutia uwekezaji mkubwa katika kubinafsisha mashirika ya umma na sasa Serikali inapata mapato makubwa kutoka sekta hii mpya (kwa mfano TBL na TCCL) na pia sekta ya madini (hasa ya dhahabu) ambayo nayo imeanza kutoa matunda na yataongezeka katika kipindi hiki kipya.

11. Malengo makuu ya Mwelekeo wa sera za CCM Katika Miaka ya Tisini yalikuwa mawili. **Kwanza mwelekeo ulitamka kuwa lengo la Ujamaa na Kujitegemea ni kuhakikisha kuwa uchumi wa Tanzania unamilikiwa na kuendeshwa na wananchi wenyewe kwa njia mbalimbali**. Hii ni sera ya msingi ambayo utekelezaji wake ni wa muda mrefu na unaohitaji mipango na mikakati thabiti.

12. Pili, Mwelekeo wa Miaka ya Tisini ulisisitiza kwamba lazima nguvu na uwezo wetu uelekezwe **kwenye kuinua kiwango cha nguvu za uzalishaji mali ili kuinua uchumi wa taifa.** Kwa sasa kiwango hicho kiko chini sana: rasilimali watu inatumia maarifa kidogo sana katika uzalishaji, zana za uzalishaji (vitendea kazi) bado ni duni sana, takriban jembe la mkono, panga, n.k. na miundo mbinu ya uzalishaji mali iko nyuma. Hivyo, kazi iliyo mbele yetu ni **kuwajenga wananchi (watenda kazi) kwa elimu na maarifa ya kisasa,**

kueneza matumizi ya zana za kisasa (vitendea kazi) na kujenga miundombinu ya uchumi wa kisasa.

13. Malengo haya makuu ya Mwelekeo wa Sera za CCM za miaka ya Tisini yanatuunganisha na majukumu ya Mwelekeo wa Sera za CCM za Miaka ya 2000 hadi 2010. Kwa kuendeleza malengo hayo mawili kazi iliyo mbele yetu ni **kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea na uwezeshaji wa kiuchumi wa wananchi**.

SURA YA PILI

KUJENGA MSINGI WA UCHUMI WA KISASA WA TAIFA LINALOJITEGEMEA

14. Uchambuzi yakinifu wa hali ya uchumi wa Tanzania ni kuwa uchumi wetu una sifa kuu mbili: ni **uchumi ulio nyuma** na **uchumi tegemezi**. Sifa hizi mbili za uchumi wetu zinategemeana. Katika hali ya sasa ya uchumi wa dunia, nchi haiwezi kujitegemea kiuchumi wakati uchumi wake uko nyuma na pia uchumi wake hauwezi kuwa ulioendelea kama haujitegemei. Kadri uchumi unavyozidi kuwa wa kisasa ndivyo nchi inavyoingia katika mkondo wa kujitegemea kiuchumi.

Uchumi Ulio Nyuma

15. Ukiondoa sekta ndogo ya kisasa ya viwanda na biashara sekta kuu ya uchumi wan chi yetu, ambayo inaajiri asilimia themanini ya wananchi na kuchangia asilimia hamsini ya GDP, ni kilimo, ufugaji na uvuvi. Kilimo, ufugaji na uvuvi wetu kwa sehemu kubwa ni wa jadi. Hali hiyo inafanya uchumi wa vijijini uendelee kuwa wa kujikimu. Uchumi wa kujikimu ni matokeo ya matumizi madogo ya maarifa yakisasa ya kanuni za kilimo bora, zana hafifu – jembe la mkono, panga, shoka n.k. – katika uzalishaji mali. Matokeo ya matumizi duni ya maarifa – kanuni za zana bora – ni wakulima kuwa na mashamba madogo madogo yasiyokuwa na tija na hivyo yasiyotoa ziada ya mazao. Ndiyo maana uchumi ulio nyuma (wa kujikimu) ndilo chimbuko la umaskini, ujinga na maradhi. Njia ya kuondokana na uchumi ulio nyuma kwa kujenga msingi wa uchumi wa kisasa unaosukumwa na maarifa ya kisasa, yaani sayansi na teknolojia.

Uchumi wa Taifa Linalojitegemea

16. Kujitegemea kama nchi siyo kujitosheleza kwa kila mahitaji ya nchi. Kujitegemea ni kwa nchi kujijengea uwezo wa ndani wa kiuchumi na utaalam wa kugharamia mahitaji ya lazima kwa ustawi na maendeleo ya taifa. Nchi kujitosheleza kwa chakula ni jambo zuri hasa pale ambapo kama ilivyo kwa Tanzania ni nchi yenye ardhi tele na rutuba.

17. Hata hivyo jambo la msingi kwa nchi ni kuwa na uwezo wa kiuchumi wa kuzalisha bidhaa kwa ajili ya mahitaji ya ndani na kuuza ziada ya bidhaa kwa wingi katika soko la dunia ili kupata uwezo wa fedha za kigeni za kulipia mahitaji ya bidhaa kutoka nje kwa ajili ya soko la ndani. Ni muhimu kusisitiza tena kuwa nchi ambayo sehemu kuu ya

uchumi wake ni wa kujikimu haiwezi kuzalisha ziada kubwa ya bidhaa za kuuza nje na kuiwezesha kujitegemea. Hivyo kuondokana na hali ya uchumi ulio nyuma ndio ufunguo wa kujitegemea kwa nchi.

Mkakati wa Kujenga Msingi wa Uchumi wa Kisasa wa taifa linalojitegemea

18. Mtazamaji mtafiti wa Tanzania atabaini yafuatayo:- Watanzania wanaishi katika mkanganyiko wa mambo. Matumizi yetu na mahitaji yetu mengi ni ya kisasa, mavazi, usafiri, huduma za jamii kama elimu na afya, mahakama, ulinzi na usalama, barabara, mawasiliano yote haya ni ya kisasa (yaani kilimo, ufugaji na uvuvi) ni wa kujikimu ambao vitendea kazi vyake vikuu ni jembe la mkono na zana nyingine za jadi. Ni wazi kuwa hali hii ni ya mgongano wa kimsingi. Lazima mgongano huu wa hali upatiwe suluhisho.

19. Uzoefu wa dunia unaonyesha kuwa huduma za kiuchumi na za kijamii za kisasa: barabara, mahakama, elimu, afya, maji n.k. zote zinagharamiwa na uchumi wa kisasa. Hivi ndivyo ilivyo Ulaya, Marekani n.k. na hakuna mgongano. Nchi za Asia ambazo mara nyingi tunazitolea mifano zimeelewa hilo na wamechukua na wanaendelea kuchukua hatua za kuufanya uchumi wao uwe wa kisasa zaidi ili umudu kubeba gharama za huduma za jamii, mahakama, barabara n.k. kutokana na misaada na mikopo kutoka kwa wahisani. Hili si jawabu la kudumu. Jawabu la kudumu ni kujenga nguvu za uchumi wetu za kulipia gharama hizo za lazima za maendeleo yetu.

Mkakati Wenyewe: "Modenaizesheni"

20. Katika azma ya kujenga msingi wa uchumi wa kisasa (Modenaizesheni) wa taifa linalojitegemea msukumo wetu uelekezwe kwenye maeneo yafuatayo:-

ELIMU YA KISASA

21. Elimu ina nafasi ya msingi pale nchi inapoamua kujiletea mapinduzi ya kiuchumi na kijamii. Uchumi wa kisasa unahitaji watenda kazi wenye maarifa yanayohusu kanuni na pia maarifa ya kumudu vitendea kazi vya aina mbali mbali. Lazima watu hawa waandaliwe kwa kupewa elimu inayohitajika. Msukumo wa elimu ya kisasa katika kipindi hiki ujielekeze kwenye:

(i) Elimu ya kawaida ya Awali, Msingi, Sekondari, Chuo Kikuu
(ii) Elimu ya Ualimu
(iii) Elimu ya Ufundi
(iv) Elimu ya watu Wazima yenye manufaa
(v) Elimu ya Uchumi wa Soko, maarifa ya biashara na uwekezaji na uendeshaji wa shughuli za kisasa.

22. Elimu ya watu wazima yenye manufaa (functional education) ikiandaliwa vizuri ina uwezo wa kutoa mchango mkubwa katika kujenga uchumi wa kisasa katika sekta nyingine hasa za kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji madini na pia afya n.k. katika muda mfupi. Umuhimu wake uzingatiwe katika mapana hayo.

KILIMO, UFUGAJI NA UVUVI WA KISASA

23. Kilimo cha kisasa ndio ufunguo wa maendeleo ya uchumi wote wa nchi yetu. Kilimo cha kisasa kitaongeza tija na kutoa ziada kubwa. Hatua kwa hatua uchumi wa kujikimu utatoweka na badala yake kujengeka uchumi wa soko wa kisasa. Ongezeko la tija na ziada ya mazao litakuwa na matokeo ya kupungua kwa umaskini uliokithiri vijijini na pia nchi itakuwa na mazao mengi na bora ya kuuza nje na kujipatia fedha nyingi za kigeni. Ongezeko la mapato ya wakulima litawawezesha kumiliki/kutumia zana za kisasa zaidi na hivyo kuwawezesha kuongeza ukubwa wa mashamba yao ambayo kwa sasa ni madogo mno.

24. Mkakati wa mapinduzi ya kilimo uwe na malengo makubwa yafuatayo:-

(i) Kuwawezesha wakulima kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao kwa kila eka kulingana na viwango vya kisasa kwa zao linalohusika.
(ii) Kuwawezesha wakulima kuongeza ukubwa wa maeneo wanayolima.
(iii) Kuwakaribisha na kuwavutia wakulima wa kati na wakubwa.

25. Njia za kufanikisha malengo hayo hapo juu ni pamoja na:-

(i) Serikali kutazama upya wajibu wake wa kuwaandaa na kuwapanga maafisa ugani ili waweze kuwafikia wakulima kwa karibu. Maafisa ugani hawa wanahitaji kupigwa msasa wa mwelekeo na pia kupewa motisha.

(ii) Wakulima wasaidiwe kujenga upya vyama vyao vya ushirika vya msingi na kuwasaidia waanzishe vyama vya kuweka na kukopa.
(iii) Mipango ya ufundishaji wa ng'ombe wa kilimo ifufuliwe na ienezwe kwenye Wilaya zenye mazingira muafaka.
(iv) Suala la kueneza kilimo cha matrekta litafutiwe mkakati
(v) Mfumo muafaka wa **upatikanaji wa pembejeo** na mfumo muafaka wa **masoko ya wakulima** iwekwe.
(vi) Vituo vya utafiti wa kilimo vifufuliwe
(vii) Kila zao kubwa liandaliwe utaratibu (package) utakaoainisha malengo ya pembejeo, upanuzi wa kilimo cha zao, ongezeko na wingi wa zao na soko.
(viii) Kilimo cha maua na matunda kipewe msukumo pia.

26. Kilimo cha kisasa kiendane na uhakika wa maji. Pamoja na kuendelea kutegemea mvua kwa sehemu kubwa na kwa muda mrefu ujao, lazima tuendelee na miradi midogo midogo na mikubwa ya umwagiliaji maji. Serikali iandae miundombinu ya umwagiliaji na wananchi wawezeshwe kuyatumia majaluba yaliyoandaliwa na kuendesha wenyewe mradi kwa msingi wa ushirika wao.

Ufugaji Bora

27. Pamoja na maendeleo ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ambayo yamepatikana hasa katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha (hasa Arumeru), Kagera na Mbeya (Rungwe), eneo la ufugaji nchini bado liko nyuma. Ng'ombe, mbuzi na kondoo peke yao wanapata milioni thalathini, ng'ombe wakiwa nusu ya hao. Lakini wanyama hao wana uzito wa wastani ambao ni mdogo, pia wanatoa maziwa kidogo. Hivyo yapo mambo ya msingi ambayo itabidi yafanyike ili sekta hii ielekee kwenye usasa:-

(i) Lazima majosho yaliyopo yafufuliwe na mapya yajengwe.
(ii) Uandaliwe mfumo wa kufikisha pembejeo zinazohitajiwa na wafugaji
(iii) Iwekwe mipango ya kueneza mbegu bora za mifugo
(iv) Wataalam wa mifugo washauriwe na wawezeshwe kuingia kwenye ufugaji wa kisasa
(v) Uandaliwe mkakati wa kitaifa wa kuwaundia wachungaji wahamaji mazingira yatakayowahakikishia kupatikana kwa maji, malisho na majosho ili hatua kwa hatua waondokane na maisha ya kuhama hama.
(vi) Uandaliwe mfumo muafaka wa masoko ya mazao ya mifugo.
(vii) Malambo yafufuliwe na mapya yajengwe.

(viii) Wananchi wahimizwe na kuwezeshwa kuingia kwenye ufugaji wa kati na mkubwa wa kibiashara,

(ix) Wakaribishwe wawekezaji wakubwa katika ufugaji.

Uvuvi

28. Uvuvi unadumaa katika pwani ya bahari na kwenye maziwa makuu hasa kwa sababu ya zana duni. Mradi maalum wa uvuvi katika Ziwa Tanganyika umetoa matunda mazuri. Katika kipindi hiki itafaa kutafuta njia ya kuanzisha miradi kama ule wa Kigoma katika maeneo mengine. Katika mipango yetu ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi suala la mikopo kwa wavuvi ili wajipatie zana za kisasa itabidi lipewe uzito. Katika kipindi hiki, itabidi hatua zichukuliwe za kudhibiti uvuvi holela unaofanywa na meli za kigeni kwenye bahari kuu ndani ya mipaka yetu. Aidha, ziimarishwe hatua za kudhibiti uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira ya bahari na maziwa makuu.

VIWANDA

29. Sekta ya Viwanda ndiyo hasa chimbuko la sekta ya kisasa. Mapinduzi ya viwanda ya Ulaya ndiyo yaliyoibua uchumi wa kisasa. Uchumi wa viwanda una nguvu kubwa ya kuziingiza sekta nyingine za uchumi katika mkondo wa uchumi wa kisasa. Wenye kujua mambo ya uchumi wamewahi kusema kuwa **kilimo ndio msingi wa uchumi na viwanda ndiyo sekta kiongozi ya uchumi**.

30. Nchi yetu si nchi ya viwanda. Sekta ya viwanda Tanzania ingali ndogo sana na mchango wake kwenye pato la taifa ni kama asilimia kumi tu. Lakini ili tuitekeleze azma yetu ya kujenga msingi wa uchumi wa kisasa basi lazima sekta hii ipewe uzito unaostahili. Vinginevyo tutakwama katika utekelezaji wa modenaizesheni katika maeneo mengine.

31. Jitihada zetu katika kipindi hiki cha Mwelekeo wa Sera za Chama tuzingatie kazi zifuatazo:-

(i) Kushughulikia ufufuaji wa viwanda vilivyopo nchini hasa vyanguo, ngozi, kanvasi, usindikaji wa mazao ya kilimo, mbao, madawa n.k. kwa kuwakaribisha wawekezaji.

(ii) Kufufua na kuimarisha viwanda na miundombinu ya utengenezaji wa vifaa na mitambo ya chuma kwa kushirikisha wawekezaji.

(iii) Kutoa kipaumbele kwenye suala la Utafiti na Maendeleo (R&D) na kuweka mtandao bora wa vituo/taasisi za R & D nchini

pamoja na kuviwezesha kuyafikisha matokeo ya utafiti kwenye soko.

(iv) Kutafuta wawekezaji wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga kwa lengo la kuipatia nchi yetu msingi wa viwanda mama.

(v) Kuipa SIDO nguvu mpya ya kueneza viwanda vidogo kama ilivyokuwa huko nyuma.

(vi) Kubuni mpango wa kuwaandaa mabingwa katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia ya viwanda humu nchini na ng'ambo.

MADINI

32. Tanzania inaaminika kuwa na utajiri mkubwa wa madini. Kwa miaka mingi sekta hii ilikuwa ya wachimbaji wadogo wasio na zana za kisasa. Machimbo ya almasi ya Mwadui ndiyo yaliyokuwa makubwa na ya kisasa. Hali imebadilika sasa ya dhahabu Nzega, Kahama na Geita. Serikali iendelee kuwakaribisha wawekezaji wakubwa katika sekta hiyo ya madini.

33. Kazi nyingine iliyo mbele yetu katika kipindi hiki ni kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo kwa mambo yafuatayo:-

(i) Mipango ya kuwawezesha kupata zana za kisasa

(ii) Wapatiwe elimu ya kisasa ya madini, uchimbaji na masoko duniani

(iii) Uwekwe mfumo ulio wazi wa soko la madini la humu humu nchini.

34. Pamoja na kwamba wachimbaji wadogo wadogo wa madini hupata fedha za kutosha kuwawezesha kuinua hali zao za maisha, ukweli ni kuwa wengi wao wana tabia ya kufuja mali kila wanapopata. Matokeo ni kuwa wengi wao pamoja na mapato mazuri wanayoyapata bado wanabaki katika hali ya umaskini. Iko haja ya kubuni utaratibu wa ushauri nasaha kwa wachimbaji madini wadogo wadogo ili waanze kutumia fedha wanayochuma kwa busara zaidi.

UTALII

35. Tanzania ina utajiri mkubwa wa maliasili ambazo ni vivutio kwa watalii wa ndani na nje. Sekta ya utalii inajitokeza kutoa mchango mkubwa katika ukuaji na upanuzi wa uchumi wa nchi yetu. Katika miaka kumi ijayo tujielekeze kwenye kuimarisha ubora wa huduma

kwa watalii Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na kupanua uwezo wa kuwapokea watalii wengi zaidi na kuongeza udhibiti wa mapato ya utalii.

36. Pamoja na kuendelea kuwavutia watalii wa kigeni iko haja sasa ya kupanga taratibu za kuwavutia watalii wa ndani ili nao waonje mazingira mema ya maliasili ya nchi yao. Iko pia haja ya kuongeza nafasi na kuweka mikakati thabiti kwa Watanzania kushiriki katika kutoa huduma kwa watalii.

37. Maliasili inayovutia ni maeneo yale ambayo hayajachafuliwa. Kwa hiyo jitihada za kuvutia watalii ziambatane na jitihada za kuhifadhi mazingira katika mbuga za wanyama, misitu, fukwe za bahari na maziwa n.k.

MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI

38. Ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa lazima uambatane na ujenzi wa miundombinu ya kisasa. Miundombinu ya kisasa ni pamoja na:-

    (i) Barabara za kisasa za lami na changarawe.
    (ii) Reli, Viwanja vya Ndege, bandari
    (iii) Mawasiliano ya kisasa

        (a) Simu
        (b) Posta
        (c) Kompyuta
        (d) Vyombo vya habari

    (iv) Nishati – Umeme, petroli na gesi
    (v) Maji ya nyumbani, ya viwandani na ya umwagiliaji mashamba.

    Miundombinu hii ikiwa na matatizo makubwa jitihada za kujenga uchumi wa kisasa zitakwama.

39. Kwa upande wa nishati, Tanzania imekwishagundua gesi nyingi Songo Songo, Kilwa na pia Mnazi Bay, Mtwara. Mradi wa Songo Songo umekwishaanza kutekelezwa. Wakati huo huo jitihada zinaendelea za kutafuta petroli. Kipindi hiki cha miaka kumi kitumike kuendeleza jitihada hizi kwa kushirikiana na wawekezaji.

SERA MUAFAKA ZA FEDHA NA BIASHARA

40. Katika ulimwengu wa sasa wa biashara isiyo na mipaka, itabidi ziwekwe sera muafaka za fedha na biashara zitakazohakikisha ushiriki mzuri wa Tanzania katika mwelekeo huo, bila ya kuathiri uwezo wake na kuishi kama taifa linalojitegemea. CCM ihakikishe kwamba Serikali zinaweka sera zitakazoiwezesha Tanzania kufaidika na matunda ya muafaka yatakayotokana na biashara isiyo na mipaka na kujikinga na taathira zake. Aidha, ni muhimu kwa Serikali kupiga vita biashara ya magendo na vitendo vya biashara visivyo vya haki.

KAZI, MAARIFA, NIDHAMU, IDADI YA WATU NA MAENDELEO YA UCHUMI

Kazi, Maarifa na Nidhamu

41. Kiwango na kasi ya maendeleo ya watu katika fani mbalimbali hutegemea utamaduni wa kazi walio nao watu wa jamii inayohusika. Jamii ya watu wasiothamini kazi, wavivu na wazururaji, maendeleo yake hudumaa. Jamii ya watu wachapa kazi, wenye juhudi, jamii hiyo hupiga hatua katika maendeleo. Azma yetu ya kujenga msingi wa uchumi wa kisasa itafanikiwa tu iwapo tutatimiza sharti hili la kwanza la maendeleo kwa kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye kazi, Watanzania wote wenye uwezo huo wafanye kazi.

42. Sharti la pili la maendeleo ni maarifa. Katika kufanya kazi mbalimbali binadamu hupata maarifa yaani hugundua kanuni zinazotawala maumbile na hujiundia vitendea kazi (zana) vinavyomrahisishia kazi yake. Kwa kutumia kanuni za maumbile na zana bora katika kufanya kazi, kazi huwa na tija, ufanisi na ziada kubwa. Kazi isiyoambatana na maarifa haina tija, ufanisi na ziada kubwa. Jamii inayoendesha shughuli zake bilaya maarifa, maendeleo yake si endelevu. Maendeleo endelevu hupatikana pale ambapo watu katika jamii husika wanatumia maarifa katika kufanya kazi. Uchumi wa kisasa ni uchumi wa kazi na maarifa. Azma yetu ya kujenga msingi wa uchumi wa kisasa lazima iambatane na mapinduzi katika mtazamo wa wananchi wetu kuhusu kazi na maarifa. Tunahitaji kujenga utamaduni wa kuthamini maarifa na ubunifu katika kazi.

43. Kazi na maarifa lazima kuambatana na nidhamu. Kila aina ya kazi ina kanuni zake. Utekelezaji wa kanuni katika kufanya kazi kwa maarifa ndiyo nidhamu. Kwa upande wa viwanda na mitambo nidhamu ya kazi imejengeka katika mpangilio na mtitiriko wake. Mashamba makubwa ya kisasa huendeshwa kwa nidhamu ya aina za

viwandani. Nchi yetu ni ya wakulima wadogo wadogo. Pamoja na kuhimiza juhudi za kazi na maarifa itabidi kusisitiza pia nidhamu katika kilimo, ufugaji na uvuvi. Watu hawawezi kwenda mashambani saa zozote wapendazo. Katika mazingira ya nchi yetu, kilimo makini kinafanyika asubuhi na saa za jioni. Aidha, ubora wa kazi ni muhimu lakini muda wa saa za kazi ni muhimu pia. Mtu aliyelima vizuri kwa saa tatu tu kila siku atavuna mazao pungufu kuliko mazao ya aliyelima vizuri kwa saa sita kila siku katika msimu wa zao hilo hilo. Lazima sasa tusisitize nidhamu katika kazi na matumizi ya maarifa na muda unaotumika katika kazi.

Idadi ya watu na Maendeleo ya Uchumi

44. Pamoja na kuhimiza kazi, maarifa na nidhamu ili kuongeza tija, ufanisi na ziada katika uchumi kuna suala la idadi ya watu na maendeleo ya uchumi. Kaya yenye watu wanane wanapolima na kuvuna chakula cha kuwatosha watu watano tu kwa mwaka, kaya hiyo itaishi kwa dhiki bila maendeleo. Lakini kaya yenye watu wane ikilima na kuvuna chakula cha kutosheleza mahitaji ya watu tisa, kaya hiyo itakuwa na ziada ya chakula cha watu watano ambacho kikiuzwa kitaipa kaya uwezo wa kujiletea maendeleo kwa kupanua shamba na kuongeza pembejeo, kusomesha watoto, kununua bati n.k. Familia hii itakuwa inaondokana na umaskini hatua kwa hatua kutokana na ziada inayozalishwa.

45. Kwa taifa ni hivyo hivyo. Ili taifa lipige hatua za maendeleo lazima ukuaji wa uchumi wake uongezeke kwa kasi kubwa kuliko ongezeko la idadi ya watu nchini. Katika Tanzania idadi ya watu inaongezeka kwa asilimia tatu kwa mwaka wakati uchumi uakua kwa asilimia nne. Ukuaji wa uchumi wa asilimia nne ni mdogo mno kuleta maendeleo ya kuridhisha nchini kwani robo tatu ya ongezeko linafutwa na ongezeko la idadi ya watu la asilimia tatu. Ili kupata maendeleo ya haraka na endelevu lazima ukuaji wa uchumi wa Tanzania ufikie kati ya asilimia sita na kumi kwa miaka kadhaa mfululizo. Jambo hili tuna uwezo nalo tukitoa kipaumbele kwenye hatua za kilimo cha kisasa kilichoainishwa hapo juu na pia kwa kueneza uzazi wa mpango. Kilimo cha kisasa kitaongeza ziada ya chakula na mazao ya biashara na uzazi wa mpango utadhibiti ongezeko holela la idadi ya watu.

Akiba na Maendeleo ya uchumi

46. Uchumi wa kisasa, pamoja na kwamba unategemea kazi na maarifa lakini unachochewa sana na mtaji. Mtaji ni mali ya akiba ambayo imehifadhiwa kwa thamani ya fedha. Mtaji ni muhimu katika

kusukuma uchumi kwa kuwa unawezesha kupatikana kwa mitambo, mashine na zana nyingine na kuwawezesha watu kuajiriwa katika shughuli za uchumi.

47. Nchi yenye limbikizo kubwa la akiba (mtaji) ina uwezo mkubwa wa kutumia akiba au mtaji huo kuwekeza katika uchumi wake. Nchi yenye limbikizo dogo la akiba katika vyombo vyake vya fedha itakuwa na uwezo mdogo wa kuwekeza katika uchumi wake. Nchi nyingine za Afrika ikiwemo Tanzania zina asilimia ndogo ya akiba katika mifumo yao ya uchumi hivyo uwezo wao wa kuwekeza katika uchumi kutokana na nguvu za ndani ya nchi ni mdogo.

48. Ziko sababu kadhaa zinazofanya nchi zetu ziwe na akiba kidogo: uzalishaji duni wenye tija za ziada kidogo; wananchi kutokuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba; tabia iliyoenea nchini ya kufuja mali katika sherehe za harusi, ngoma, starehe n.k., faida za makambpuni ya nje kupelekwa ng'ambo, matajiri wa Kiafrika kupeleka akiba zao kwenye mabenki ya Ulaya n.k.

49. Mapambano ya kujenga msingi wa uchumi wa kisasa lazima yaambatane na jitihada za kitaifa za kukuza akiba nchini ili uwekezaji katika uchumi uongezeke kwa kutumia nguvu zetu za ndani na kuungwa mkono na mitaji ya wawekezaji wa kutoka nje. Wananchi waelimishwe juu ya umuhimu wa kujiwekea akiba katika vyombo vya fedha kwa faida yao binafsi na kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu.

SURA YA TATU

MIKAKATI YA UWEZESHAJI WA KIUCHUMI WA WANANCHI

50. Mwelekeo wa Sera za CCM katika Miaka ya Tisini uliweka lengo la msingi la Sera za CCM pale ulipotamka:-

> "*Lengo la Ujamaa na Kujitegemea katika miaka ya tisini litakuwa kuhakikisha kwamba wananchi wenyewe wanamiliki na kuendesha uchumi wa nchi yetu, mmoja mmoja, kwa kupitia vyama vyao huru vya ushirika wa aina mbalimbali, kwa kupitia makampuni ya wananchi ya ubia ambamo maelfu ya wananchi watanunua hisa na kwa kupitia umilikaji wa dola kwa mashirika yote yatakayoendelea kuwa mikononi mwake.*
>
> *Kwa mtazamo huo wa CCM sehemu kubwa ya uchumi wa nchi inakusudiwa imilikiwe na wananchi wenyewe ili kuinua hali ya maisha yao na kutosheleza mahitaji yao ya msingi*".
>
> Hii inaendelea kuwa Sera na lengo kuu la CCM katika miaka ya 2000-2010.

51. Katika kutekeleza Sera hii imebainika kuwa kuna ugumu wa kuifanikisha kutokana na ukweli kwamba Watanzania Waafrika huko nyuma hawakupewa nafasi ya kushiriki katika uchumi wa kisasa wa kilimo, viwanda na biashara ya ndani na nje. Kwa vile Waafrika waliachwa kwenye sekta ya uchumi wa jadi wa kilimo, ufugaji na uvuvi na kuwa vibarua wa soko la sekta ya kisasa hadi leo wanaendelea kuwa pembezoni mwa sekta ya kisasa ya uchumi wa nchi yetu. Kwa ujumla hawana uwezo wa umiliki na kuendesha uchumi huo wala mitaji na uzoefu. Mkakati wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ni njia inayobuniwa kuwafanya Watanzania walio wengi nao waweze kumiliki na kuendesha uchumi katika nchi yao. Dhana kuu hapa ni **uwezeshaji**, yaani kuunda mazingira muafaka yatakayowapatia fursa za kumiliki ardhi, viwanda na zana za kazi, kupata mitaji ya kuwekeza katika shughuli za kiuchumi, kupata elimu na maarifa ya kuendesha biashara na miradi ya kiuchumi, n.k. Katika utekelezaji wa mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, vijana na wanawake wapewe kipaumbele.

Ushirika Kama Chombo cha Uwezeshaji

52. Silaha ya wanyonge ni umoja. Katika eneo la uchumi na hasa katika kilimo, ufugaji na uvuvi, ushirika ndicho chombo kikuu cha kuwaunganisha wahusika na kuwapa nguvu ya kutetea maslahi yao na kujiendeleza.

53. Ushirika katika kilimo, ufugaji na uvuvi ni chombo cha kuwapatia mtaji kutokana na michango na ushuru, njia ya hakika ya kufikisha mazao kwenye masoko, njia ya hakika ya kuwafikishia wahusika pembejeo na zana za ushirika ni mkondo wa kueneza elimu ya ushirika na elimu ya uzalishaji bora kwa wanachama wake.

54. Kwa kutumia ushirika huko nyuma katika mikoa ya Ziwa (hasa Kagera), Kilimanjaro na Mbeya iliwezekana kuwasomesha watoto wa wakulima katika shule za ndani na nje na hivyo kuchangia katika maendeleo ya maeneo hayo.

Tujenge Upya Ushirika wa Msingi

55. Kutokana na kuvurugika kwa ushirika nchini kwa kuenea kwa wizi, ubadhirifu na uozo wa rushwa ndani ya mfumo huo, iko haja ya ushirika kujengwa upya. Mkazo uwekwe kwenye kujenga upya ushirika wa vyama vya msingi. Ushirika wa msingi imara utawasaidia wakulima, wafugaji na wavuvi kuondokana na umaskini. Wananchi wengi zaidi washawishiwe kujiunga na ushirika huu, wana CCM wakiwa mstari wa mbele katika kuonyesha mfano.

Tueneze Ushirika wa Kuweka na Kukopa

56. Ushirika wa kuweka na kukopa ni chombo cha uhakika cha ukombozi wa kiuchumi kwa wanyonge, wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyakazi pia. Umuhimu wa ushirika wa aina hii haujaeleweka na viongozi wengi nchini. CCM itabidi itoe msukumo mkubwa juu ya elimu ya ushirika na juu ya manufaa ya ushirika wa kuweka na kukopa katika kuwapatia wahusika mtaji ili waweze kushiriki katika uwekezaji nchini.

Mifuko ya Mikopo ya Kuwawezesha wananchi Kiuchumi

57. Tatizo kubwa linalowakuta wananchi walio wengi wanaoamua kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi ni kutokuwa na mitaji. Katika kutafuta njia ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mitaji kwa njia za mikopo mifuko mbalimbali imebuniwa.

58. Serikali Kuu imekuwa ikitenga fedha za mikopo kwa wanawake, vijana na wafanyabiashara. Serikali za Mitaa zimekuwa zikitenga asilimia kumi ya makusanyo yao kwa ajili ya mikopo ya wanawake na vijana. Mikopo hii itabidi iendelezwe na, utaratibu uimarishwe. Fedha zinazotengwa na Serikali Kuu ni muhimu pia ziwe na mtiririko wa uhakika na kiwango kinachotengwa kiongezwe.

59. NGOs nazo zimejitokeza katika jukumu la kutoa mikopo ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Mifano ya NGOs hizi ni Poverty Africa, Pride Tanzania na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote. Pia kuna mfuko wa N.I.G.P., mfuko wa Rais wa Zanzibar na Mifuko ya Wahisani.

60. Katika miaka kumi ijayo itatubidi kuunda mazingira mazuri zaidi yatakayowavutia watu wa ndani na wa nje wenye uwezo wa kuanzisha mifuko ya mikopo ya kuwawezesha waanchi kiuchumi. Bado mahitaji ya mitaji midogo midogo ni makubwa nchini. Aidha, mifuko hiyo ielekezwe pia vijijini.

Vyombo vya Fedha na Benki za Wananchi

61. Tanzania iko nyuma katika kuanzisha vyombo vya fedha vyenye lengo la kutoa mikopo ya kuwawezesha wananchi kuingia katika miradi ya kisasa ya kilimo, ufugaji, uvuvi au viwanda. Vyombo vya fedha vya aina hii vitahitajika sana katika kipindi hiki. Micro-Finance Bank inatazamiwa kutoa mchango mkubwa katika eneo hili.

62. Kuanzishwa kwa mabenki ya wananchi kunaunda mazingira mazuri ya kuchochea maendeleo. Jiji la Dar es Salaam linachukua hatua za mwisho za kukamilisha uanzishaji wa benki ya Wananchi wa Dar es Salaam. Wanaushuirika katika Mkoa wa Kilimanjaro wamekwisha kuanzisha benki yao ya ushirika. Wananchi wa mikoa mingine wahamasishwe ili nao waanzishe benki za wananchi.

Upendeleo kwa Wananchi Katika Ajira na Biashara

63. Wajibu mkubwa wa dola ni kuhakikisha kuwa nafasi ya kwanza ya ajira na biashara nchini iwe imetengewa Watanzania. Pale tu

ambapo hakuna Watanzania wenye elimu na uwezo wa kuimudu kazi ndipo wageni wafikiriwe. Vile vile katika biashara sehemu kubwa ya biashara za reja reja zinaweza kufanywa na Watanzania wenyewe. Kwa mfano, hakuna sababu ya kuwaachia wenye miradi mikubwa ya kutotoa vifaranga washindane kwenye soko la reja reja na wananchi wafugaji wadogo wadogo wa kuku.

64. Wakati umefika wa kuweka mazingira bora ya upendeleo kwa Watanzania kulingana na yanayofanyika katika nyanja za kimataifa. Biashara ni kazi, hivyo biashara ambazo Watanzania wanaziweza basi watengewe wao.

65. Aidha iko haja ya kuendelea kuwashirikisha Watanzania katika ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma yaliyobaki, katika utoaji wa zabuni za Serikali na za kimataifa na katika mashindano ya biashara mbalimbali yanayoendeshwa nchini Tanzania.

66. Mipango iandaliwe ya kuhamasisha ubia kati ya wawekezaji wa kigeni na wananchi wa Tanzania.

Mafunzo ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi

67. Watanzania walio wengi hawana maarifa na uzoefu wa kuendesha shughuli za uchumi wa kisasa. Kwa sababu hiyo, mipango ya kuwawezesha wananchi kiuchumi lazima iambatane na mipango ya elimu na mafunzo juu ya menejimenti ya aina mbalimbali za uchumi wa kisasa. Elimu na ujuzi ndivyo vitakavyowawezesha kushiriki katika ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa.

68. Wakati huo huo, itabidi iwepo mipango ya kuwaandaa Watanzania wenye vipaji hivyo katika fani za uongozi wa uchumi na kuandaa watu ambao wako tayari kuthubutu kuchukua hatua za kiuchumi. Kuthubutu kiuchumi ndiyo chimbuko la msukumo katika uchumi wa kisasa. Hatuna Watanzania wengi waliojitokeza katika fani hii hivi sasa. Lazima tuwatafute na tuwaandae.

Msukumo wa Maendeleo Vijijini

69. Ili kuunda mazingira ya kuwawezesha wananchi wa vijijini kiuchumi hatua za kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii ziongezwe. Barabara za vijijini ni muhimu kwa kuchochea maendeleo ya uchumi. Bidhaa zitayafikia masoko kwa urahisi na binadamu watawasiliana kwa wepesi. Kwa upande mwingine huduma za jamii zilizoboreshwa

zitachangia katika kuwashirikisha wananchi katika ujenzi wa uchumi na kuimarisha vita dhidi ya umaskini.

70. Kipindi hiki kinahitaji maandalizi ya sera mpya ya maendeleo vijijini inayozingatia jukumu kuu tulilojipa la kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Maendeleo vijijini maana yake ni mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi, kufuta umaskini na ujinga na kuboresha afya, kueneza mawasiliano bora na barabara, kueneza umeme n.k. Yote haya kwa pamoja yanahitaji ainisho la kisera kuhusu maendeleo vijijini.

SURA YA NNE

SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

71. Hatua kubwa imefikiwa na nchi yetu katika kujenga mtandao wa msingi wa kuhakikisha wananchi wetu hasa walio vijijini wanapata huduma za msingi za jamii. Kutokana na hali mbaya ya kifedha iliyozikabili Serikali zetu katika miaka ya themanini na tisini, sehemu kubwa ya upanuzi wa mtandao huo ilitegemea nguvu za wananchi na pia ubora wa huduma za jamii ulipungua.

72. Kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano inafanya kazi kubwa ya kulipa madeni yetu na hatimaye Wahisani wamekubali kuyasamehe mengi yake chini ya mpango wa kuzisamehe nchi maskini zinazodaiwa sana (HIPCs), CCM haina budi kushauri na kuhakikisha unafuu huo unatumika kwa ukamilifu kuongeza ubora wa huduma za jamii na kuendelea kupanua mtandao wa huduma hizo.

Huduma za Elimu

73. Ili elimu yetu iwe kweli nyenzo ya msingi katika jitihada za kujenga uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea na kuwawezesha kiuchumi wananchi haina budi ipewe mwelekeo wa kukuza ubunifu na mbinu za kutatua matatizo, na kujenga utamaduni wa matumizi ya sayansi na teknolojia kuanzia katika ngazi za chini. Aidha, mwelekeo huo uzingatie falsafa ya msingi ya Elimu ya Kujitegemea.

74. Katika kuzikabili gharama kubwa za utoaji wa elimu hasa katika mwelekeo huu mpya, itabidi Serikali ziongeze kipaumbele katika bajeti ya elimu na pia kuimarisha zaidi ushirikiano ("partnership") na wahsani, sekta ya binafsi na jamii kupitia vyombo na taasisi zake mbalimbali (k.v. NGOs, Jumuiya za Wananchi, n.k.). Aidha, itabidi jitihada ziongezwe za kuwaelimisha wazazi juu ya jukumu lao la msingi la kuchangia gharama za elimu ya watoto wao na kuweka utaratibu wa kuwasaidia wale wasiokuwa na uwezo.

75. Malengo ya msingi ya upanuzi na uboreshaji wa huduma ya elimu yatakuwa:-

    (a) Kuifikisha elimu ya awali kwa wote wanaostahiki haraka kadri itakavyowezekana.
    (b) Kutoa elimu bora ya msingi kwa wote wanaostahiki ifikapo 2010.

(c) Kuzipatia shule za sekondari zinazojengwa na wananchi vifaa na walimu na kuongeza nafasi kwa wasichana.

(d) Dola kuelekeza nguvu zaidi katika maandalizi ya walimu wa ngazi zote.

(e) Kurekebisha mfumo wetu wa utoaji wa elimu ya juu kwa kuboresha matumizi ya fursa zilizopo na zitakazoongezwa ili wanafunzi wengi zaidi waweze kupata nafasi. Utekelezaji wa lengo hili utahitaji ubunifu wa hali ya juu na kujifunza kutokana na uzoefu wa nchi nyingine.

(f) Kupanua na kuimarisha elimu ya ufundi na biashara ili kusaidia juhudi za ujenzi wa uchumi wa kisasa.

Elimu ya Watu Wazima

76. Katika kuzipa msukumo jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi na kujenga uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea, elimu ya watu wazima itabidi ipewe uhai mpya na mfumo mzima wa utoaji wa elimu hiyo urekebishwe ili ulenge kwenye kutoa elimu yenye manufaa. Kwa kuzingatia umuhimu wa sayansi na teknolojia Serikali itabidi iweke katika mfumo wake wa elimu ya watu wazima kipaumbele katika kuendeleza maarifa ya kisasa yatakayowasaidia wahusika kuboresha kazi zao wanazozifanya. Lengo ni kusukuma kilimo cha kisasa, ufugaji wa kisasa, uvuvi wa kisasa na kadhalika ili kuwawezesha wananchi kupata kipato zaidi na kuongeza pato la taifa pamoja na kujenga na kuimarisha utamaduni wa maendeleo ya sayansi na teknolojia katika jamii.

Elimu ya Ufundi

77. Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kutoa umuhimu katika upanuzi na uimarishaji wa elimu ya ufundi kwa lengo la kupanua maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia itakayochochea na kuchangia katika ujenzi wa uchumi wa kisasa unaojitegemea.

Afya

78. Sera ya CCM katika kipindi kijacho itaendelea kusisitiza upatikanaji wa huduma muhimu za afya kwa wananchi wote bila ya ubaguzi. Aidha mkazo uwekwe katika kinga dhidi ya maradhi, kupambana na maradhi ya milipuko, huduma maalum kwa mama na mtoto na usambazaji wa elimu ya afya kwa jamii. Aidha wananchi watahamasishwa ili waendelee kuchangia gharama za afya.

79. UKIMWI ni tishio kubwa kwa uhai wa taifa letu. Kwa hiyo, taifa lielekeze nguvu zake katika kupambana na UKIMWI. Pamoja na UKIMWI juhudi pia zitaelekezwa kwenye kuendeleza mapambano dhidi ya magonjwa makubwa ya hatari kama vile malaria, kifua kikuu na magonjwa ya kuhara.

Huduma za Maji

80. Chama Cha Mapinduzi kitaendelea na juhudi zake za kuhimiza Serikali zitekeleze malengo na majukumu yanayoainishwa katika Sera ya maji Tanzania. Mambo yatakayoendelea kusisitizwa ni pamoja na kuwawezesha wananchi kupata maji safi, salama na ya kutosha kwa matumizi yao karibu na sehemu wanazoishi. Mahitaji ya mifugo, kilimo, viwanda na umeme pia itabidi yapatikane kutokana na mipango ya utekelezaji wa sera hiyo.

81. Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhimiza uimarishaji na upanuzi wa teknolojia ya ukingaji na utumiaji wa maji ya mvua mijini na vijijini, uchimbaji, usafishaji naufufuaji wa malambo; na mamlaka za maji za ngazi mbalimbali zitapaswa kushirikisha nguvu za wananchi wenyewe katika usambazaji wa huduma za maji. Aidha, suala la ulinzi na hifadhi ya mazingira katika vyanzo vya maji litapewa msukumo maalum. Kamati za maji vijijini ziimarishwe na kuenezwa.

Makaazi

82. Kwa lengo la kuondokana na matatizo ya upungufu mkubwa wa nyumba za kuishi mijini na uduni wa nyumba hizo vijijini, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi hiki kitaelekeza Serikali ziandae mikakati ya jinsi ya kuyapatia ufumbuzi matatizo hayo. Wananchi watahamasishwa na kuhimizwa kujenga nyumba bora. Kwa upande wa mijini Serikali zijiongezee uwezo wake wa kupima viwanja, maendeleo na upanuzi upangwe kwa kutumia maarifa ya kisasa. Aidha, wawekezaji wahamasishwe watakaojihusisha na utengenezaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba za kuishi. Wananchi wenyewe wahamasishwe ili wajijengee nyumba bora mijini na vijijini. Jitihada za kuongeza uzalishaji katika uchumi ili kubresha maisha ya wananchi mijini na vijijini lazima ziende sambamba na ujenzi wa nyumba bora za kuishi.

SURA YA TANO

UTAWALA BORA, DEMOKRASIA NA MADARAKA YA WANANCHI

83. Kazi ya kubadili mfumo kutoka mfumo wa Chama kimoja na kuingia mfumo wa vyama vingi vya siasa ilitekelezwa kwa ufanisi mkubwa katika miaka ya tisini hadi kupelekea nchi yetu kufanya Uchaguzi Mkuu mwaka 1995 katika mazingira mapya katika hali ya amani na utulivu.

84. Kazi kubwa ya CCM katika kipindi cha miaka kumi ijayo (2000 hadi 2010) ni kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuimarisha misingi ya demokrasia kwa kuhakikisha kuwa shughuli zote za kisiasa zinawashirikisha wananchi wote kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi bila kuacha mianya ya kujengeka kwa udikteta wa aina yo yote. Lengo la kuimarisha na kupanua demokrasia ni kuweka mazingira ambayo hatimaye yatachangia kwa kiasi kikubwa kusisimua maendeleo ya uchumi wa nchi yetu.

Serikali na Utawala

85. Uzoefu tuliopata katika miaka ya tisini umedhihirisha umuhimu wa utawala bora ambao ni utawala unaozingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Aidha, utawala wa demokrasia ni sehemu muhimu ya utawala bora. CCM itawajibika kuendelea kuimarisha demokrasia na utawala bora ndani ya Chama na kuendelea kuzitaka Serikali ziimarishe utawala wa sheria na kuzipitia upya sheria zinazogongana kwa lengo la kuimarisha demokrasia na utawala bora katika jamii. Kwa lengo hilo, Serikali ziimarishe utawala wa sheria na kuzipitia upya sheria zinazogongana kwa lengo la kuiondoa migongano hiyo. Aidha, mambo ambayo yamekuwa yakifanywa kwa maagizo yawekewe mfumo wa sheria.

86. Utawala bora katika nchi yetu uambatane na mambo yafuatayo:-

    (a) **UWAZI** katika kuendesha masuala ya nchi ikiwa ni pamoja na matumizi mazuri ya fedha na raslimali.

    (b) **UFANISI** katika kufanya maamuzi na kusimamia utekelezaji wake.

(c) **UADILIFU** katika utendaji kwa kuzingatia misingi ya sheria na kanuni za utendaji kazi.

(d) **UWAJIBIKAJI** kwa wananchi ili waweze kudhibiti jinsi nchi yao inavyoendeshwa na watendaji kazi Serikalini.

(e) Utawala wa sheria, kanuni na taratibu.

87. Tangu miaka ya themanini CCM ilijijengea utaratibu mzuri wa kubadilisha uongozi kwa amani, utulifu na mshikamano wa hali ya juu. CCM itaendelea kudumisha utamaduni huu kwa faida ya Taifa letu.

Serikali za Mitaa

88. Uzoefu umedhihirisha umuhimu wa Serikali za Mitaa kama chombo cha wananchi cha kuwashirikisha katika utawala wa umma. Katika miaka ya tisini zimefanyika juhudi za makusudi za kuimarisha uhusiano baina ya Halmashauri za Serikali za Mitaa, Watendaji wa Halmashauri na Wananchi ili kuongeza uwajibikaji zaidi wa Halmashauri hizo kwa wananchi. CCM itahakikisha kuwa uwajibikaji huo kwa wananchi unaongezeka.

89. CCM inaipongeza Serikali ya awamu ya tatu kwa kuanzisha Mpango wa uboreshaji wa Serikali za Mitaa. Pamoja na kuziwezesha Serikali za Mitaa kutoa huduma bora za jamii mpango huo usisitize pia kuziwezesha Serikali za Mitaa kuwa kichocheo cha maendeleo ya wakazi wa maeneo yao na kufuta umaskini. Lazima tujenge Serikali za Mitaa zinazowajibika.

Vyombo vya Habari

90. Katika miaka ya 2000 hadi 2010 CCM itapaswa kuhakikisha kuwa Serikali inalinda uhuru wa wananchi wa kujipatia habari kwa kuhakikisha kuwa vyombo vilivyopo vinaendelea kushindana ili kutoa huduma iliyo bora kwa ufanisi wa hali ya juu kwa mujibu wa sheria. Taasisi zinazosimamia sekta ya habari na mawasiliano zitapaswa kupewa uwezo zaidi wa kuhakikisha kuwa kila anayeingia katika ushindani huo anazingatia viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. Jumuiya za waandishi wa habari zinazowajibika zitiwe moyo.

Vyama vya Wafanyakazi

91. Kutokana na ubinafsishaji wa mashirika mbalimbali yaliyokuwa yanamilikiwa na Serikali kumejitokeza kukua kwa kasi kubwa kwa sekta ya binafsi ambayo ndiyo inachukua nafasi ya kuwa mwajiri mkubwa badala ya sekta ya dola. Wakiwa chini ya sekta binafsi wafanyakazi wanahitaji kuwa na umoja wenye nguvu ya kutetea maslahi yao. Umoja huu utapatikana ndani ya vyama vyao huru. Aidha, mabaraza ya wafanyakazi katika bodi ni hatua muhimu ya kupanua demokrasia mahala pa kazi. CCM itapaswa kuhimiza ushirikishwaji wa wafanyakazi uwekewe mazingira mazuri na kupanuliwa kwa lengo la kuwapa wafanyakazi kauli kubwa zaidi na kwamba suala la ushirikishwaji wa wafanyakazi sasa liwe la kisheria.

92. CCM itaendelea kuhimiza uhuru wa wafanyakazi wa kujiunga na vyama huru vya wafanyakazi vilivyoanzishwa kwa mujibu wa sheria ili kutetea maslahi yao.

Vyama vya Ushirika

93. Vyama vya ushirika vina sura mbili. Kwa upande mmoja vyama hivyo ni vyombo wanavyotumia wanachama kwa ajili ya maendeleo yao ya kiuchumi. Kwa upande wa pili vyama hivyo ni vyombo ambavyo huwapa fursa wanachama wake kushiriki moja kwa moja au kwa njia ya uwakilishi kuviendesha vyama hivyo na kutoa maamuzi mbalimbali kwa manufaa yao ya kimaendeleo. Kutokana na sura hii ya pili ambapo wanachama wanakuwa karibu na vyama vyao katika kuviendesha ndiyo maana vinakuwa ni vyombo muhimu vya upanuzi wa demokrasia ndani ya umma.

94. Kwa kutambua umuhimu wa vyama vya ushirika kama vyombo muhimu vya kidemokrasia katika umma, CCM katika miaka ya 2000 itapaswa kuhakikisha kwamba Serikali inasimamia kwa dhati utekelezaji wa sera ya maendeleo ya ushirika.

95. Mambo muhimu ambayoCCM itapaswa kuyazingatia na kuyasimamia kwa nguvu zote katika kipindi hiki ni pamoja na kuhakikisha kuwa elimu ya ushirika inawafikia wana ushirika wote kwa lengo la kuwafanya waelewe vizuri misingi, kanuni na taratibu za ushirika. Uelewa huo utawawezesha wanaushirika kuwa na uhuru wa kuchagua viongozi wanaowataka wao wenyewe, kushirikishwa wanachama katika maamuzi kuhusu uendeshaji wa vyama vyao na menejimenti na halmashauri kuwajibika kwa wanachama.

Jumuiya za Wananchi

96. Mageuzi ya kisasa yalifanyika katika miaka ya tisini yaliweka mazingira ya kuimarika kwa Jumuiya za Wananchi (NGOs na CBOs) zilizokuwepo na kuchipuka nyingine nyingi ambazo kwa jumla zinalenga katika kutetea maendeleo ambayo wananchi wanayaona yanawafaa katika maeneo yao.

97. Katika kipindi hiki cha miaka ya 2000, CCM pamoja na Serikali zake wataendelea kuhamasisha wananchi kuimarisha jumuiya hizi kwa lengo la kupanua wigo wa wananchi wa kujiletea maendeleo yao kwa kutumia makundi mbalimbali kwa mujibu wa sheria na bila ya kuathiri mshikamano wa kitaifa.

Jumuiya Nyingine za Wananchi

98. CCM itaendelea kuunga mkono nafasi ya Jumuiya nyingine za wananchi zikiwemo za kiuchumi kama vile vyama vya wafanyabiashara, au kitaalam zikiwemo za walimu, madaktari, wahandisi, waandishi wa habari au za kijamii kama vile za wanawake, vijana na vikundi vya maendeleo vya wananchi.

SURA YA SITA

MAENEO MAALUM

Hifadhi ya Mazingira

99. Uchambuzi wa kitaifa katika suala zima la uharibifu wa mazingira hapa nchini umebainisha matatizo yanayohitaji suluhisho la haraka kama taifa linataka kupata maendeleo endelevu kwa kutumia maliasili zilizopo sasa. Matatizo hayo ni pamoja na uharibifu wa ardhi, kutopatikana kwa maji safi kwa wakazi wa mijini na vijijini, uchafuzi wa mazingira kwa jumla, upotevu wa makazi ya viumbe na bayoanuwai katika nchi kavu na majini na uharibifu wa misitu.

100. Katika miaka ya hivi karibuni, Serikali iliweka mikakati maalum ya kupambana na tatizo hili. CCM itaendelea kuhakikisha kuwa Serikali zinaendelea kutekeleza kwa kasi zaidi mikakati ya kukabili uharibifu wa mazingira na kuongezeka kwa umaskini.

101. Kampeni ya upandaji miti iliyozinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano mwezi Aprili, 1999 iendelezwe na kusimamiwa kote nchini.

Vita Dhidi ya Rushwa

102. Juhudi za kupambana na uozo wa rushwa nchini zimeanza kutoa matunda. Kazi ya kupambana na vitendo vya rushwa ni kazi ya kudumu na inahitaji uongozi uliojitolea muhanga kupambana na vitendo hivyo.

103. Kwa kuzingatia uzito wa tatizo lenyewe, CCM itahakikisha kuwa Serikali zinaendelea na mapambano hayo kwa kasi kubwa zaidi, na kwa kuwashirikisha wananchi.

SURA YA SABA

UTAMADUNI NA MICHEZO

Utamaduni

104. Hivi sasa nchi yetu imo katika kujenga utamaduni imara ambao utakabiliana na misukosuko itokanayo na uchumi huria na kunufaika na matunda ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Chama Cha Mapinduzi kitaendeleza harakati za kuenzi na kulinda mila na desturi nzuri na kuzitokomeza mila na desturi mbaya. Katika kujenga na kuendeleza utamaduni bora na endelevu CCM itatilia mkazo elimu kwa wote. Elimu ndiyo nyenzo thabiti ya kurithisha yote yaliyo mema katika jamii yetu kwa vizazi vipya. Aidha, elimu ndiyo itakayowawezesha Watanzania kuyatambua mazuri ya tamaduni nyinginezo duniani na kuyatumia kuinua ubora wa maisha yao, na wakati huo huo kujikinga na athari za tamaduni za nje zinazodhalilisha utamaduni na utu wa Mtanzania.

105. Fani ya sanaa ni moja ya nyenzo kubwa zilizotumiwa katika harakati za kudai uhuru wa nchi yetu na katika kuongeza kasi ya maendeleo ya jamii. Chama Cha Mapinduzi kitahimiza matumizi ya sanaa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo na uhuru wetu. Aidha, Chama kitahimiza matumizi ya sanaa katika kampeni za kupambana na matatizo makubwa ya kitaifa kama vile umaskini, ujinga, UKIMWI na kuleta ulingano wa jinsia. CCM itazitaka Serikali zake kuelekeza nguvu katika maandalizi mazuri ya uwanda wa sanaa ili uwe ni kioo cha mwenendo mzuri wa maisha ya wananchi na pia chanzo cha kipato kizuri kwa wasanii wenyewe.

Michezo

106. CCM inatambua na itaendelea kutambua umuhimu mkubwa wa michezo katika kujenga afya ya miili na akili. Kwa ajili hiyo CCM itaendelea kutilia mkazo mkubwa suala la kuendeleza michezo yote nchini ikiwa ni pamoja na michezo ya jadi.

SURA YA NANE

SIASA YA MAMBO YA NJE

107. Siasa ya mambo ya nje ya nchi yo yote ni kielelezo cha siasa na hali ya ndani ya nchi hiyo. Tanzania ni nchi iliyo nyuma na tegemezi kiuchumi. Tumeamua kuondokana na hali hiyo. Katika miaka kumi kuanzia sasa tumeamua kuelekeza nguvu zetu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisiasa wa taifa linalojitegemea. Kwa mantiki hiyo, Sera za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa tutahakikisha zinatusaidia kuchochea mafanikio ya jitihada hizo za ndani za kujenga msingi imara wa uchumi wa kisasa na huduma bora za jamii.

108. Aidha, kuimarisha na kuendeleza utawala bora, demokrasia na haki za binadamu ni malengo ya kipaumbele tuliyoviwekea katika kipindi hiki sambamba na jitihada za kujenga uchumi. Kwa maana hiyo, uhusiano wa Kimataifa ulenge katika kutuunganisha na wenzetu duniani wenye malengo kama hayo, utuwezeshe kubadilishana uzoefu, kujenga mshikamano na ushirikiano katika kulinda na kuendeleza malengo hayo yanayotuunganisha na kudumisha amani na utulivu katika dunia.

109. Tanzania wakati wote imesisitiza kuwa silaha ya wanyonge ni umoja. Umoja wa taifa umejengwa kwa kuzingatia ukweli huo. Kutokana na sera ya ndani ya umoja, tumeweza kutetea na kuendeleza umoja katika uhusiano wa kimataifa kwa kuanzia na sera ya ujirani mwema, uanzishaji wa ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki na wa nchi za SADC na kuwa katika mstari wa mbele kuendeleza malengo ya umoja wa Nchi za Afrika (OAU). Malengo haya lazima yaendelezwe katika kipindi hiki kipya.

110. Kutokana na hayo hapo juu, Siasa ya mambo ya nje na uhusiano wetu wa Kimataifa usisitize yafuatayo:-

    (a) Sera ya Mambo ya Nje ilenge katika kuiletea Tanzania maslahi ya kiuchumi kwa:-

        - Kuwavutia na kuwakaribisha nchini wawekezaji makini
        - Kuvutia sayansi na teknolojia mpya nchini
        - Kuwavutia watalii

    (b) Sera ituwezeshe kushiriki katika kuendeleza haki, utawala bora na demokrasia katika dunia, kuendeleza

ushirikiano baina ya mataifa na amani duniani. Wakati huo huo tuendelee kutetea haki za binadamu na kupiga vita udhalimu popote ulipo.

(c) Lazima tuendelee na sera ya ujirani mwema na kuimarisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Jumuiya ya SADC, Umoja wan chi za Afrika (OAU) na Umoja wa Mataifa (UNO).

(d) Sera ya mambo ya nje ilenge katika kulitangaza jina la nchi yetu na kuijengea Tanzania heshima miongoni mwa mataifa.

SURA YA TISA

ULINZI NA USALAMA

111. Sera za CCM kuhusu ulinzi na usalama zitaendelea kulenga kwenye mambo ya msingi yafuatayo:-

(a) Kujenga Jeshi la ulinzi la Wananchi wa Tanzania lililo dogo na la kisasa; jeshi imara katika utayari na utendaji kivita; maafisa na wapiganaji wazalendo na waadilifu; na jeshi linaloshirikisha wananchi wenyewe katika kutekeleza majukumu ya kulinda taifa kwa kupitia ulinzi wa mgambo.

(b) Kujenga jeshi la usalama wa raia dogo na lenye utaalam wa kisasa wa kudhibiti machafuko katika jamii, mbinu za kisasa za upelelezi na umahiri katika kuendesha mashtaka; jeshi ambalo ni rafiki wa raia wema na tishio kwa wahalifu; jeshi lenye uzalendo na uadilifu.

(c) Jeshi la Kujenga Taifa na jeshi la Kujenga Uchumi ambayo ni chuo cha uzalendo na ulinzi kwa vijana; chuo cha kuwaandaa vijana katika uzalishaji mali na ufundi, chuo cha kuimarisha umoja na usawa wa Watanzania.

SURA YA KUMI

CHAMA CHA MAPINDUZI NA UMOJA WA TAIFA; AMANI NA UTULIVU NA MAPINDUZI YA UCHUMI

112. Miaka ya hamsini katika karne ya ishirini ilishuhudia kuibuka kwa vyama viwili vya siasa katika Tanganyika na Zanzibar na viongozi wawili nyota ya karne kwa eneo letu la Afrika. Chama cha TANU chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kiliendesha mapambano ya kupigania uhuru kwa umahiri mkubwa na kufanikiwa kunyakua uhuru wa Tanganyika kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza kwa muda mfupi wa miaka sita, yaani toka 1954 hadi 1961. Chama cha ASP, chini ya uongozi wa Sheikh Abeid Amani Karume, kiliendesha mapambano ya kupigania uhuru na hatimaye kufanikiwa kuipindua Serikali haramu ya Sultani wa Waarabu wachache tarehe 12 Januari, 1964 miaka saba tangu ASP iundwe Februari 2, 1957.

113. Kutokana na imani yao kubwa katika umuhimu wa umoja wa Afrika, viongozi hawa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume waliasisi Jamhuri ya Tanzania kwa kuunganisha Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar Aprili 26, 1964. Hatimaye, tarehe 2 Februari vyama vya Tanganyika African National Union na Afro Shiraz Party viliungana na kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kutokana na kuuawa kwa Sheikh Abeid Amani Karume kulikofanywa na wahaini wa taifa mwaka 1972 kuasisiwa kwa CCM kulifanywa kwa ridhaa ya TANU ikiongozwa na Mwalimu J.K. Nyerere na ya ASP ikiongozwa na Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi.

114. Tunapoingia katika karne ya ishirini na moja na melenia ya tatu Watanzania tuna wajibu wa kutafakari urithi wa kitaifa tunaorithishwa na karne iliyopita ya ishirini. Tumeibuka katika karne ya ishirini na moja Tanzania ikiwa nchi huru na taifa huru. Ukoloni na Utawala wa Sultani wa Kiarabu ni historia. Tanzania ni nchi moja yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumerithi kutoka karne iliyopita Tanzania yenye umoja wa kitaifa, udugu na mshikamano unaopigiwa mfano katika Afrika na kutambuliwa katika mabaraza ya kimataifa. Waasisi wa taifa letu, Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere na Makamu wake wa kwanza, Sheikh Abeid Amani Karume wameturithisha nchi yenye amani na utulivu. Mpaka alipoaga dunia ukingoni mwa karne ya ishirini Baba wa Taifa alitazamia kuiona Tanzania ikiingia katika karne hii ya ishirini na moja ikiwa nchi huru, jamhuri (moja) ya Muungano wa Tanzania, taifa lenye umoja, udugu na mshikamano na nchi yenye amani na utulivu.

115. Katika kutafakari ibara tatu zilizotangulia na jukumu kuu (central task) tulilojipa katika Mwelekeo huu wa Sera katika miaka kumi ijayo majukumu makubwa ya CCM katika kipindi hiki kipya yanajitokeza kuwa matatu yafuatayo:-

(a) **CCM iwe Mhimili wa umoja wa Taifa na wa Muungano**

Zimeanza kujitokeza dalili kwamba wanasiasa uchwara katika baadhi ya vyama vya siasa wanapandikiza mbegu za udini, ukabila na hisia nyingine zinazowatenganisha Watanzania. Lengo la wanasiasa uchwara hawa ni kupandia udini, ukabila, n.k. ili kupata madaraka ya kisiasa bila kujali madhara makubwa kwa taifa yanayoambatana na sera hizo za kibaguzi.

TANU na ASP na CCM chini ya uongozi wa waasisi wake ndivyo vyama vilivyoujenga umoja wa Taifa. Wanachama ndio wamekuwa kichocheo cha umoja, udugu na mshikamano wa Watanzania. Uongozi wa CCM uwaongoze wana CCM katika vita dhidi ya sera zote za ubaguzi wa Watanzania kwa misingi ya dini, kabila, eneo, jinsia, n.k. Wana CCM tupinge makanisa, misikiti au mahekalu kutumiwa kama vituo vya kuandikisha wanachama wa vyama vya siasa; kuwachagulia waumini vyama bora ama vyama visivyofaa n.k.

Ili CCM iendelee kuwa na nguvu ya mhimili wa umoja wa taifa, lazima ihakikishe kuwa sarakani ya udini, ukabila na ubaguzi wa aina nyingine yo yote haijipenyezi ndani ya CCM yenyewe. CCM ambayo imeingiliwa na uozo wa udini na ukabila haitaweza kuongoza mapambano ya kuimarisha umoja, udugu na mshikamano wa Watanzania. Wana CCM wanaoendekeza au kupandikiza ubaguzi ndani ya chama chetu lazima wafichuliwe na kuchukuliwa hatua.

(b) **CCM Idumishe Amani na Kutoa Uongozi kwa Taifa**

Mwalimu J.K. Nyerere, Baba wa Taifa, aliwahi kusisitiza "*Pasipokuwa na haki hapawezi kuwa na amani*". Tanzania imefanikiwa kuwa nchi yenye amani na

utulivu kutokana na sera zake zinazoweka mbele uhuru, haki, usawa na utu. Lazima CCM iendeleze sera hizi kwa nguvu zote.

Katika kipindi cha sasa cha uchumi wa soko ambapo kuna mwelekeo wa watu wachache kulimbikiza mali kwa wingi na wananchi walio wengi kuachwa kwenye kingo za umaskini, ni muhimu kwa CCM kujitokeza wazi wazi upande wa wanyonge. CCM lazima ionekane kuwa ndilo chimbuko la sera za kuwawezesha wananchi kiuchumi kama inavyoainishwa katika Mwelekeo huu wa sera za chama chetu. Wananchi wakati wote wanataka kumjua nani ndiye kiongozi wao siyo katika mambo ya vyama tu bali hasa katika mambo ya maendeleo yao kiuchumi na kijamii.

Aidha, inapotokea kwamba taifa linakabiliwa na jambo kubwa linalokera, linaloweza kuhatarisha umoja na mshikamano wa nchi, wananchi hutegemea mtu au taasisi ijitokeze kulipatia jambo hilo tata ufumbuzi kwa maslahi ya taifa zima. Katika kipindi hiki kijacho CCM iendelee kutegemewa na Watanzania kuchukua nafasi hiyo ya uongozi kwa taifa zima. Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa ziendeleze msimamo thabiti wa **kulinda na kutetea maslahi ya chama** dhidi ya maslahi ya ubinafsi **na maslahi ya taifa** dhidi ya maslahi ya vikundi vya kibinafsi. Hivi ndivyo CCM itajijengea uhalali wa kuwa chama kiongozi kwa taifa.

(c) **CCM Kuongoza Ujenzi wa Uchumi wa Kisasa na Kuutokomeza Umaskini**

Wajibu mkuu wa tatu wa CCM katika kipindi hiki cha miaka kumi ni kuongoza ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Katika tathmini iliyofanywa na Halmashauri Kuu ya Taifa mwaka 1998 ilibainika kuwa chama chetu kilionyesha upungufu katika kutekeleza Ilani ya CCM ya 1995. Chama chenyewe hakikuainisha majukumu yake katika kutekeleza Ilani hiyo. Hivyo, hakikuweza kutoa uongozi wa kiutekelezaji na kuchangia katika utekelezaji wa jumla unaofanywa na Serikali. CCM iliridhika na wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa Serikali na kutoa kauli juu ya utekelezaji.

Mwelekeo wa Sera wa miaka ya 2000 hadi 2010 umeainisha jukumu kuu la taifa kuwa ni "*kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea*". Kazi hii ni nzito na inahitaji uongozi thabiti wa vitendo wa Chama na Serikali zake. Serikali itabidi ziyaelewe na kuyaainisha majukumu yake na kuyatafsiri katika programu mbalimbali. Chama nacho itabidi kifanye hivyo pia.

Chama kinaweza kuongoza kwanza kwa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Serikali kwa kupitia Bunge (Wabunge wa CCM), Baraza la Wawakilishi (Wawakilishi wa CCM) na Halmashauri za Serikali za Mitaa (Madiwani wa CCM).

Njia ya pili ya chama kuongoza ni kwa kupokea taarifa za utekelezaji wa Serikali, kujadili na kutoa ushauri wa Serikali. Katiba ya CCM imeweka utaratibu wa vikao vya Halmashauri Kuu ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya hadi Kata na Tawi kuwasilishiwa taarifa hizo za Serikali kwa ngazi hizo.

Njia ya tatu ni ya umuhimu wa kwanza. Hii ni ya kuongoza kwa kutekeleza. WanaCCM wakulima waongoze kwa wao wenyewe kutekeleza mapinduzi ya kilimo katika mashamba yao, kwa mazao wanayolima. Kwa upande wa ufugaji bora wanaCCM wafuagaji watekeleze maelekezo ya ufugaji bora wa ng'ombe wao. Wana-CCM watekeleze ushirika kwa kuwa wanachama wa chama/vyama vya ushirika. Wanachama wote wa CCM wakifanya hivyo, nchi nzima itahamasika na kuunga mkono harakati za kujenga msingi wa uchumi wa kisasa na kuangamiza umaskini.

Huko nyuma, CCM tumekuwa wazito katika kuongoza kwa kutekeleza wenyewe. Sasa tunahitaji mapinduzi katika fani hii. Kuongoza ni kuonyesha njia.